MASOMO YA KILIMO

# Kulima na Kufuga kwa Njia za Kisasa



## 100. MAELEZO

MKL
S484
.5
K8

Inades-Formation

## Masomo ya Kilimo: Hatua ya Kwanza

SNAL - SUA / O
064877 4

# 100. MAELEZO

SUA LIBRARY
SPECIAL COLLECTION

**INADES-formation**

Masomo yako ya hatua ya kwanza yamo kwenye vijitabu tisa kama ifuatavyo:

100. Maelezo

## KUHUSU UDONGO NA MIMEA

101. Jinsi ya kufahamu ardhi ifaayo
102. Jinsi ya kutayarisha shamba
103. Jinsi ya kulima
104. Jinsi ya kupanda
105. Jinsi ya kutunza shamba lako
106. Jinsi ya kuilinda mimea yako
107. Jinsi ya kuvuna

## KUHUSU UFUGAJI

108. Kulisha na kuhifadhi wanyama
109. Uzazi na magonjwa ya wanyama

Twatoa shukrani za dhati kwa shirika la "Le Cardinal Léger et ses Oeuvres (Canada)" ambalo lilitoa msaada ili kijitabu hiki kichapishwe.

© 1987 INADES-FORMATION

**Ni marufuku kunakili, kutafsiri, au kuyatoa yaliyomo katika kijitabu hiki kwa njia yo yote, katika nchi yo yote, bila idhini iliyoandikwa.**

# MPANGO WA KIJITABU CHA 100

Vifungu

**Utangulizi** .......................................... 1 - 3

Sehemu ya Kwanza: **Masomo Haya Yana Lengo Gani?** .. 4 - 5

Sehemu ya Pili: **Masomo Haya Yatakufaa Nini?** ........ 6 - 20

*Sababu ya 1: Ulimwengu Unabadilika*............ 6 - 13

*Sababu ya 2: Kilimo Kinabadilika*.............. 14 - 16

*Sababu ya 3: Kazi ya Ukulima Yahitaji Utaalam*... 17 - 20

Sehemu ya Tatu: **Muda wa Masomo** ............... 21 - 26

Sehemu ya Nne: **Jinsi ya Kujifunza** ................ 27 - 37

*Kama Unajifunza Ukiwa Peke Yako*............ 27

*Kama Unajifunza Kwenye Kikundi* ............ 28 - 30

*Yampasayo Kiongozi wa Kikundi*.............. 31 - 37

Sehemu ya Tano: **Kazi za Mazoezi** ................ 38 - 51

*Jinzi ya Kufanya Kazi za Mazoezi* ............. 38 - 47

*Kutuma Majibu Kwetu*..................... 48 - 51

1. Kijitabu kidogo hiki kina mambo ya msingi.
Yafaa ukisome kabla hujaanza kujifunza.

Kinakueleza mambo matano muhimu:

a. Masomo haya yatamsaidia na kumfaidi nani?
b. Zipo faida gani katika kujifunza?
c. Yakupasayo kujua juu ya masomo haya.
d. Jinsi ya kujifunza masomo haya.
e. Jinsi ya kufanya kazi za mazoezi.

2. Masomo haya yamepangwa kwenye mafungu manne.
Ukimaliza kujifunza masomo ya fungu moja
na kujibu vema maswali yake,
utapata barua ya kukupongeza.
Ukimaliza kujifunza masomo yote kabisa
na kujibu vema maswali,
utapata *cheti* au *shahada.*

**Cheti hiki ni ushahidi tu kuwa umejifunza masomo bora kabisa kuhusu kilimo na ufugaji.**

Huwezi kukitumia cheti hiki kutafuta kazi.

3. Utaona kuwa kila kifungu kina namba yake.
Kwa mfano, sasa unasoma kifungu cha 3.

Namba hizi zitakusaidia wakati unapojifunza.
Zitakuwezesha kupata kifungu fulani upesi
unapotaka kujikumbusha jambo fulani.

Kwa mfano: kama mnazungumza juu ya
njia mpya za kufanya kazi zenu shambani
mkitaka kujua mahali pa kusoma,
mtahitaji tu kutafuta kifungu namba 15.

Hiyo itakuwa kazi rahisi
kuliko kuambiwa mfungue ukurasa wa 7
karibu na katikati yake.





## MASOMO HAYA YANA LENGO GANI?

4. **Kwa wakulima:**

**Ukiwa Mwanamume, au mwanamke; mzee, au kijana, kama umeamua kuwa mkulima,**
masomo haya yatakusaidia
uielewe kazi yako vema,
uzalishe mazao mengi na bora zaidi,
uyauze kwa njia ifaayo,
ili maisha yako yawe bora zaidi
na jamaa yako ipate furaha kubwa,
ili kijiji chote kisitawi zaidi
na nchi nzima iwe na maendeleo
makubwa na ya kupendeza zaidi.

5. **Kwa viongozi:**

**Ukiwa mshauri, mwalimu au kiongozi wa shughuli za kilimo,**
masomo haya yatakusaidia kukumbuka
mambo mengi ambayo umeshajifunza.
Yatakuonyesha njia za kueleza maarifa mapya
kwa lugha nyepesi itakayomsaidia mkulima.

**Ukiwa kiongozi wa aina yo yote kijijini,
au mwalimu shuleni, au mtaalam,
au ukiwa msimamisi wa kikundi cho chote
kinachoshughulika na mambo ya ukulima,
utayafaidi masomo haya.**
Kama unataka ufaulu zaidi katika kazi yako,
ukitaka kupata furaha kubwa zaidi
katika kuwatumikia wananchi
ambao ni ndugu zako hapo kijijini,
kama unataka kuijenga nchi yako vema zaidi,
masomo haya yatakufaa wewe hasa.

## SEHEMU YA PILI

## MASOMO HAYA YATAKUFAA NINI ?

## SABABU YA KWANZA: ULIMWENGU UNABADILIKA


6. **Miji inapanuka. Inakuwa na watu wengi.**

Mwaka wa 1968 mji wa Nairobi ulikuwa
na watu nusu milioni.
Sasa una karibu watu milioni moja.

Mwaka wa 1968 mji wa Dar es Salaam
ulikuwa na watu 300,000 tu.
Lakini sasa una watu 800,000 hivi.

Mji wa Kampala nao ulikuwa na
watu 352,000 mika kumi iliyopita.
Leo watu karibu 700,000 wanaishi Kampala.

**Ndivyo miji yetu yote inavyokua haraka.**




**Watu wanaoishi mijini hawana mashamba.**
**Lakini wanahitaji chakula kila siku.**



7. **Pia wapo watu wengi wanaoishi katika vijiji.**

Baadhi yao hawalimi wala kufuga.
Wapo walimu wanaofundisha shuleni,
wengine ni wauguzi wanaowasaidia wagonjwa,
pia wapo mafundi wa aina nyingi
vilevile wapo watumishi na viongozi
wanaowatumikia wananchi katika vijiji.

Hawa wote pamoja na jamaa zao
wanahitaji chakula kila siku.

8. **Nchi yetu inahitaji viwanda vingi zaidi.**

Baadhi ya viwanda hivi vinahitaji bidhaa
kutoka kwa wakulima.

Fikiri juu ya viwanda vya kutengeneza
nguo, vyakula vya mikebe,
viatu na vyombo vya ngozi, vinywaji,
unga na hata aina za madawa.
Vyote vinamtegemea mkulima.

9. **Nchi za nje pia hununua mazao yetu.**


Pengine ni kwa sababu
mazao kama hayo hayastawi kule kwao.
Mazao haya ni kama pamba, mkonge,
kahawa, chai, korosho, pareto ...
Pengine ni kwa sababu
watu wa nchi hizo hawalimi
mazao ya kutosha mahitaji yao
kwa mfano, nyama, nafaka, matunda ...

Nchi za nje hununua bidhaa zinazotokana
na kazi za wakulima wetu.

10. **Mkulima mwenyewe ana mahitaji mengine.**

Anahitaji nguo, viatu na vyombo vya nyumbani.
Anahitaji nyumba bora,
baiskeli na vifaa vya kilimo.

## MKULIMA ANAHITAJI BAISKELI




Pia anahitaji kujua mambo yanayotokea
nchini kwake na ulimwenguni kote.
Kwa hivyo anahitaji radio, magazeti na vitabu.
Mambo haya yote hayapatikani bila fedha.

11. **Nchi yetu, mkoa, wilaya na kijiji**
pia vina mahitaji mapya.
Wananchi wanahitaji barabara na madaraja,
vituo vya afya na dawa za kutosha,
vyombo vya mawasiliano kama
magari, simu, posta, reli na eropleni.
Pia serikali na mashirika yake
yana watumishi wengi wanaohitaji kutunzwa.

12. **Mambo yote haya yanahitaji fedha.**
Sehemu ya fedha hii hupatikana
wakati mazao yanaponunuliwa
na nchi za nje.

13. **Mkulima ni mtu mashuhuri sana.**
**Dunia nzima inamtegemea**
**kwa chakula na bidhaa za viwandani.**
**Mkulima na nchi yake**
**huhitaji fedha zaidi na zaidi**
**ili wote waweze kupata mahitaji yao.**

*Kwa hiyo mkulima hana budi kuzalisha mazao mengi na bora zaidi.*



## SABABU YA PILI: KILIMO KINABADILIKA


14. **Kama unataka kupata**
**mazao mengi na bora zaidi,**
**imekupasa kujifunza**
**maarifa mapya ya ukulima.**

* **Maarifa mapya ya kulima,**
kupanda kwa mistari na kwa nafasi ya kutosha,
kuweka mbolea, kumwagilia maji,
na kubadili aina ya mazao.

* **Aina mpya za mbegu**
zitoazo mazao mengi na bora zaidi,
zenye kuvumilia maradhi zaidi.

* **Bidhaa za aina mpya**
Kama mbolea za chumvi chumvi
na samadi zinazoupa udongo nguvu,
madawa ya kuua wadudu na kutibu magonjwa.

* **Vifaa vya aina mpya**
kama vile vya kulimia, kupalilia,
kunyunyizia dawa, kubangulia, kutwangia,
kusagia na kusafirishia.



15. **Kama unataka kupata**
**mazao mengi na bora zaidi,**
**yakupasa kujifunza**
**maarifa mapya**
**ya kufanya kazi zako.**

* **Kuwa na kitabu cha kutunza fedha.**
Mkulima anahitaji kujua wazi
kiasi halisi cha fedha
alichopata na alichotumia.

Habari zote hizo huandikwa
kwenye kitabu cha kutunza fedha.

* **Kuchagua mazao utakayokuza.**
Mkulima anahitaji kuchagua
aina ya mazao yanayohitajika
kwa chakula cha jamaa
na pia kwa kujipatia fedha.

* **Kufanya kazi pamoja.**
Mkulima mwenye busara
hushirikiana na wenzake
hasa wakati wa kuuza mazao yake.

---

16. **Unaona sasa? Mkulima akiyafuata maarifa mapya**
**atapata mazao mengi na bora zaidi.**
**Pia atajipatia fedha nyingi zaidi.**
**Zaidi ya hayo, ataitumia fedha yake**
**kwa manufaa makubwa zaidi.**
**Yazingatie mafundisho haya kwa makini**
**kama unataka kuwa mkulima bora zaidi.**



## SABABU YA TATU: KAZI YA UKULIMA YAHITAJI UTAALAM

17. Mwuguzi anahitaji kujifunza
jinsi ya kumhudumia mgonjwa.
Kwa namna hiyo hiyo,
mkulima anahitaji kujifunza
jinsi ya kulima na kufuga.

**Ukulima ni kazi muhimu kabisa.**
Kazi ya mkulima humsaidia kila mtu:
Kila mtu anahitaji kula,
viwanda vinahitaji mazao ya kilimo,
nchi za nje hununua mazao yetu ya kilimo.


18. **Ukulima ni kazi ngumu.**

**Yakupasa kufahamu:**

* jinsi mimea inavyokua
* jinsi wanyama wanavyoishi na kuzaa
* jinsi ya kutumia bidhaa mpya
* jinsi ya kuuza mazao yako
* jinsi ya kuhesabu na kutunza fedha.

**Yakupasa pia kufahamu:**

* njia mpya za kufanya kazi yako
* aina mpya za bidhaa
* aina mpya za vifaa vya kilimo.



19. Masomo haya yana shabaha moja kubwa.
Nayo ni kumsaidia mkulima
awe na utaalam mkubwa zaidi.

Babu zetu walifanya kazi kwa shida.
Wakalima mashamba madogo kwa vijembe vidogo.
Vijana walijifunza kutoka kwa wazee wao
na kutokana na matatizo waliyokutana nayo.
Lakini hali hiyo haitoshi siku hizi.

**Yakupasa ujifunze:**

* umuhimu wa kupanda kwa mstari
* umuhimu wa kuweka mbolea
* umuhimu wa kuwapiga wanyama sindano ...

20. **Kwa kweli kujifunza masomo haya ni jambo jema.**
**Lakini litakuwa jambo la busara zaidi**
**kama ukiyafuata yote utakayojifunza.**
**Hii ndiyo sababu masomo haya**
**yanataja zaidi mazao na wanyama wako.**



## SEHEMU YA TATU: MUDA WA MASOMO

21. Masomo haya yatachukua muda mrefu.
Wakulima wengine watayakamilisha
baada ya muda wa miaka minne.
Wengine watahitaji muda mrefu zaidi,
na wengine watayamaliza upesi zaidi.
Muda utategemea bidii ya mtu.

Masomo haya yamepangwa kwa hatua 4.
Kila hatua ina vijitabu 9.

22. **Hatua ya kwanza:**

Utajifunza "kilimo na ufugaji kwa jumla".
Hivi ni kusema kuwa utajifunza
njia bora za kulima
na njia bora za kufuga wanyama.

23. **Hatua ya pili:**

Utajifunza juu ya mazao mbalimbali.
Katika hatua hii utachagua
kujifunza juu ya mazao au wanyama
fulani maalum upendavyo mwenyewe.
Utakuwa huru kuchagua vitu vinane
kutoka orodha ndefu, kwa mfano:
mpunga, mtama, kahawa, pamba, mahindi,
karanga, muhogo, chai, migomba,
kondoo, mbuzi, ng'ombe, nguruwe, kuku ...

24. **Hatua ya tatu:**

Hapa utaanza kufikiria njia za kufanya kazi:

Jinsi ya kuzalisha mazao mengi na bora zaidi,
jinsi ya kupata manufaa makubwa zaidi,
jinsi ya kutumia fedha kwa busara zaidi
ikiwa ya mkopo au kutokana na mauzo yako,
jinsi wakulima wanavyoweza kunufaika zaidi
na kuinua hali ya kijiji chao kwa pamoja.

25. **Hatua ya nne:**

Kama wewe ni **mkulima** hasa, utajifunza:

jinsi ya kutumia mbolea za chumvichumvi
jinsi ya kuchagua mbegu,
jinsi ya kunyunyizia dawa na
jinsi ya kukuza mimea uliochagua.

Kama wewe ni **kiongozi**, utajifunza:

jinsi ya kuwafikishia watu mawazo mapya kuhusu kilimo,
uchumi katika kijiji,
jinsi ya kuuza mazao ya kilimo na
jinsi ya kufanya kazi pamoja na wakulima.

26. Hapa utapata mawazo mapya ya kukusaidia kufanya kazi yako kwa njia bora zaidi.

Miaka 4 ni muda mrefu.
Hata hivyo, katika muda wa miaka 3 au 4 hivi,
utajifunza mambo mengi sana.

Labda utasema:

"Sina uwezo wa kutosha kujifunza yote hayo".

Hapo utafanya kosa.
Watu wengi kama wewe
katika nchi 20 za Afrika
wameshamaliza masomo haya.
Sasa wanafanya kazi zao za kilimo vema zaidi.

**Hata wewe waweza kufaulu kama wao.**
**Usikubali kukata tamaa hata siku moja.**



## SEHEMU YA NNE

## JINSI YA KUJIFUNZA

Kila mwaka utapata jumla ya vijitabu tisa hivi.

### KAMA UNAJIFUNZA UKIWA PEKE YAKO

27. Utajifunza yaliyomo kwenye kitabu kimoja kila mwezi.

Mwanzoni mwa kila kitabu pana maelezo kuhusu masomo yaliyomo.

Masomo ya mwezi mzima yamepangwa katika mafungu manne.
Waweza kujifunza somo moja kwa kila juma.

Mara nyingi utakuwa na kazi shambani.
Labda hutapata muda kujifunza.
Usifanye haraka.
Taratibu ndiyo mwendo.

Mara nyingine tafuta msaada.
Afisa wa kilimo, mwalimu au mkulima mwenzio, ataweza kukusaidia kama una tatizo.

Kumbuka kutunza shamba lako
na kufanya yote unayoshauriwa.
Hivyo utajifunza kwa upesi zaidi,
tena utakumbuka vema zaidi.

### KAMA UNAJIFUNZA KWENYE KIKUNDI

28. Kwa mfano, kama mnalima pamoja, mwaweza kujifunza kwa pamoja mkiwa kikundi cha wakulima.

Kujifunza kwa pamoja kwafaa sana.
Mtajifunza kwa upesi zaidi.
Mtavutwa zaidi kujifunza njia mpya
kama vile kupanda kwa mstari,
kung'oa visiki, kumwagilia maji,
kuwatumia wanyama kwenye kazi ...

Labda unafanya kazi peke yako?
Masomo haya yatakuonyesha manufaa
ya kufanya kazi pamoja na wenzako
na jinsi ya kufanya kazi pamoja.

Ikiwa umeshindwa kuwashawishi wenzako
kuanzisha umoja wa kufanya kazi,
labda mwaweza kuanzisha umoja wa kujifunza.
Ndipo mtayafaidi vema masomo haya.

29. **Je, mnataka kuanzisha kikundi cha kujifunza pamoja?**

Inawapasa:

* **Mfahamiane ya kutosha.**
Kama hamfahamiani ya kutosha
mtashindwa kuelewana mara kwa mara.

* **Kikundi kiwe na watu wachache tu.**
Kama wapo watu wengi wanaopenda
kujiunga na kikundi fanyeni hivi:
Undeni vikundi viwili au zaidi.
Watu 6 au 8 watosha kwa kikundi.

* **Fanyeni kazi kwa bidii.**
Mvivu mmoja tu
anaweza kuharibu maendeleo ya wote.

* **Chagueni Kiongozi**
Kila mshiriki awe na nafasi
kumchagua kiongozi wa kikundi.



Ikiwa yupo asiyefahamu Kiswahili
kiongozi ayatafsiri maelezo hayo
kwa lugha inayofaa.

Kiongozi asome kifungu kimoja tu.
Kisha aulize maswali.
Halafu wana kikundi waulizane
maswali wenyewe kwa wenyewe,
kwa kupeana zamu, bila fujo.
Hivyo, wote wataelewa vema.

30. **Kama ukipatwa na kuzuizi cho chote,
kwa mfano: ukiwa mgonjwa,
au ukishindwa kwa sababu yo yote,
au ukikosa kupokea somo lo lote
tuandikie barua mara moja.
Tutachukua hatua upesi kukusaidia.**

* * * * *

## YAMPASAYO KIONGOZI WA KIKUNDI

31. **Kiongozi huandaa mikutano.**
Kila juma mkutane mara moja.
Chagueni siku na saa ifaayo.
Siku hiyo na saa hiyo mkutane kila juma.
Kwa njia hiyo wengi watakumbuka.

Mikutano iandaliwe vema.
Mikutano isioandaliwa vema haifai.
Washiriki watashindwa kuzungumza,
hawataweza kuyaelewa masomo hayo.
Baada ya muda mfupi watakata tamaa.

Kwa sababu hiyo, kiongozi anapaswa
kuiandaa mikutano mapema awazavyo.

32. **Kiongozi huiongoza mikutano.**
Hutaja kwa kifupi shabaha ya somo.
Ndipo washiriki wanapouliza maswali
na kuanza kupeana mawazo kwa uhuru.

Kila mtu hujitahidi kuelewa
na kutaka kuelezwa jambo lisiloelea.
Ni wajibu wa kiongozi kuhakikisha
kuwa kila mtu anatoa mawazo yake kwa zamu.

33. **Kiongozi ana wajibu**
**kutuma majibu ya wanakikundi.**

Zipo njia tatu zifaazo hapa:

Ikiwa wanakikundi wanaweza
kusoma na kuandika,
wenyewe watajibu kwenye karatasi zao.
Yafaa wote wapewe maswali kwa wakati mmoja,
na wote watoe majibu kwa wakati mmoja pia.
Mtu apewe muda zaidi
ikiwa amezuiwa na ugonjwa au safari.
Kisha karatasi zote zitumwe kuteuliwa pamoja.

34. Ikiwa ni mwanakikundi mmoja tu
anayeweza kusoma na kuandika,
huyo atakuwa mwandishi wa kikundi.
Wanakikundi wote watajadiliana
na kutoa majibu ya maswali pamoja.
Mwandishi atayaandika majibu hayo.
Kiongozi atayatuma yote pamoja.

35. Ikiwa wanakikundi wote
hawawezi kusoma wala kuandika,
basi wamwombe mtu ye yote nje.
Huyu awasomee somo linalotakiwa.



Kiongozi wa kikundi awaongoze wote
kujadiliana na kutoa majibu
wote wakishirikiana pamoja.
Mwandishi ayaandike majibu yote
na kuyaweka mikononi mwa kiongozi.

Kwa vyo vyote ni kiongozi peke yake
aliye na madaraka ya kutuma
majibu ya maswali yote
kwa Inades-formation.

36. **Kiongozi hushirikiana na kikundi chake**
**kufikiri jinsi watakavyoyatumia**
**maarifa mapya kwenye kazi zao kijijini.**

Jambo hili ni muhimu kabisa.
Masomo haya yatakuonyesha njia mpya
za kufanya kazi shambani.
Yatumie maarifa hayo mapya uone.

37. **Mambo ya kukumbuka na hatua za kuchukuliwa:**


* Ni nani atakuwa kiongozi wa kikundi?
* Mikutano itafanyika mahali gani?
* Mikutano itafanyika siku na saa gani?

* * * * *
* * *
*

## SEHEMU YA TANO: KAZI ZA MAZOEZI

### KUFANYA KAZI ZA MAZOEZI

38. Chukua karatasi ya kwanza
yenye kazi za mazoezi.
Mfano wa karatasi hii ni huu chini.



100. MAZOEZI KUHUSU "UTANGULIZI"

ANDIKA KWA HERUFI KUBWA TAFADHALI

Jina la mwisho au ukoo: ____________

Jina la kwanza: ____________

Anwani kamili: ____________

Nambari yako ya masomo haya yote ni:

MPANGO WA TUZO

| | |
|---|---|
| I. Muhtasari | /30 |
| II. Unavyojieleza | /30 |
| III. Uchunguzi | /40 |
| JUMLA YA TUZO | /100 |

I. MUHTASARI WA SOMO

Tafadhali usiandike katika nafasi hii.

**Andika kwa herufi kubwa:**

a. Jina lako la mwisho au linalojulikana kamili.
b. Jina lako la kwanza au jina lako lingine.
c. Anwani yako kamili.

39. Tutayatazama majibu yako kwa makini.
Tutayasahihisha na kukupa mashauri.
Kisha tutakurudishia karatasi zote.
Hapo tutakupa **namba** utakayotumia.

Kila mara utaandika namba hii
kwenye karatasi zako za majibu
au kwenye barua utakazotuandikia.
Kwa njia hiyo utapata majibu upesi.

40. Kwanza soma maswali kwa uangalifu,
ndipo uanze kutafuta majibu.
Usijibu kwa haraka mno.



Kwanza andika majibu kwenye karatasi
ya vivi hivi tu.
Kisha yanakili majibu kwenye
karatasi safi utakayoituma kwetu.

41. **Yajibu maswali kwa kutumia maneno yako.**
Maneno yako mwenyewe yanapendeza zaidi
kuliko kunakili yale yaliyoandikwa kitabuni.
Usinakili majibu ya kitabu,
wala usinakili majibu ya rafiki zako.

42. Kwanza andika majibu kwenye
karatasi ya vivi hivi tu.
**Kisha soma tena maswali yenyewe.**

Je, umeyajibu maswali uliyoulizwa?
Je, umetoa majibu yasiyohusu swali?

43. **Sasa, yaandike majibu yako**
**kwenye karatasi maalum uliyopewa.**
Usiandike kupita mpaka wa pembeni.
Nafasi ya pembeni ni kwa wasahihishaji.

44. **Karatasi yenye kazi za mazoezi**
**imepangwa katika sehemu kuu tatu:**

* Sehemu ya kwanza ya mazoezi ni
**muhtasari wa somo lote.**
Unaposoma sehemu hii utatakiwa
kufanya jambo fulani.
Jambo hili litakuwa tofauti
kwa kila somo.
Tafadhali soma maelezo ya
sehemu hiyo kwa makini kila mara.

45. * Sehemu ya pili ni
**maswali kuhusu somo lenyewe.**
Yapo maswali matano hapa.
Fikiri kwa makini kabla hujayajibu.
Jibu kwa kutumia maneno yako mwenyewe.

SUA LIBRARY SPECIAL COLLECTION



064 8774

46. * Sehemu ya tatu ni
**maswali juu ya kazi yako ya kilimo.**
Haya yatakuwa juu ya hali halisi
katika shamba au maisha kijijini.

Andika ukweli mtupu.
Hapana faida kutunga majibu ya uongo.
Kumbuka kazi hii ni kwa manufaa yako
na ya watu wote katika kijiji chako.

Kabla ya kujibu, fikiri sana.
Fikiri juu ya kazi unayofanya.
Fikiri juu ya maisha ya kijiji.

Hili ni jambo muhimu kabisa.
Masomo haya yatakuzoeza
kufikiri kwa makini juu ya kazi yako.
La sivyo, hayatakufaa kitu.

47. * **Nafasi ya kuandika barua.**
Ukurasa wa mwisho wa karatasi zako
una nafasi ya kutuandikia **barua.**
Waweza kutueleza jambo lo lote
juu ya maisha na shamba lako,
mimea na wanyama wako,
matatizo au manufaa unayopata.
Tueleze kuhusu mambo mapya
unayofanya siku hizi.

**Ikiwa kuna jambo ambalo halijakuelea vema,**
**andika barua utueleze mara moja.**
**Tutajaribu tuwezavyo kukusaidia.**





48. Kabla ya kutupelekea majibu yako hakikisha
kuwa umeandika majina yako kamili
na pia namba yako uliyopewa.
Kisha uyaweke makaratasi hayo kwenye bahasha.
Anwani yetu imeandikwa mwishoni mwa kijitabu.
Hakikisha kuwa umebandika stampu
yenye thamani ya kutosha kwenye bahasha.
Mwulize afisa wa posta atakushauri.

49. **Kukurudishia makaratasi yako.**
Tutayasahihisha majibu utakayoandika
na kuyarudisha makaratasi hayo kwako.
Tafadhali uyasome mawaidha yetu kwa makini
mara ukiyapokea makaratasi yako.

Kama hukuyaelewa masahihisho yetu,
tuandikie barua utudai maelezo zaidi.
Barua hiyo ije na majibu yako yajayo.

50. Sasa utarudi shambani kulima.
Je, utalima kama ulivyolima zamani?
Utafanyaje ili ulime kwa maarifa zaidi?

51. **Jambo muhimu katika masomo haya**
**si kujibu vema maswali peke yake.**
**Masomo haya yatakuonyesha njia mpya**
**za kufanya kazi yako ya ukulima.**

---

**Ukitaka kuwa mkulima wa kisasa**
**yakupasa kufanya kazi kwa bidii.**
**Kujaza maarifa kichwani hakutoshi**
**bila kufanya kazi kwa bidii na ujuzi.**
**Hiyo ndiyo tofauti kuu kati ya**
**mkulima wa kisasa mwenye kuendelea**
**na mkulima asiyependa maendeleo.**

LEGAL DATE DUE MKL S484 .5 K8

SOKOINE NATIONAL AGRICULTURAL LIBRARY
P.O.BOX 3022 MOROGORO TANZANIA.

MKL S484 .5 K8

*Kimechapishwa na*
*Act Print Ltd., S.L.P. 48127, Nairobi, Kenya*

## VITUO VYA INADES - FORMATION

**AFRIKA YA MASHARIKI**
Inades - Formation - P. O. Box 14022, Nairobi, Kenya.

**OFISI KUU**
Inades - Formation - 08 B. P. 8, Abidjan 08, Ivory Coast.

* * * *

**BURKINAFASO**
Inades - Formation - B. P. 1022, Ouagadougou.

**BURUNDI**
Inades - Formation - B. P. 2520, Bujumbura.

**CAMEROON**
Inades - Formation - B. P. 11, Yaounde.

**CHAD**
Inades - Formation - B. P. Moundou.

**ETHIOPIA**
Agri - Service Ethiopia - P. O. Box 2460, Addis Ababa.

**IVORY COAST**
Inades - Formation - B. P. 2007, Bouake 01.

**RWANDA**
Inades - Formation - B. P. 866, Kigali.

**TOGO**
Inades - Formation - B. P. 9, Dapaon.

**ZAIRE**
Inades - Formation - B. P. 5717, Kinshasa.